# Miaka Mitatu ya Rais Samia Yaleta Ustawi na Mafanikio Makubwa katika Masoko ya Mitaji

C M S A
Capital Markets and Securities Authority



- Sekta ya Masoko ya Mitaji Imara, Himilivu na yenye mafanikio makubwa
- Tanzania yaweka ALAMA TANO za Kwanza za Mafanikio Kusini mwa Jangwa la Sahara
- Wataalamu na Taasisi zenye weledi na ujuzi kwa ngazi ya kimataifa waongezeka
- Elimu ya Fedha na Uelewa wa Masoko ya Mitaji waongezeka
- Ufanisi wa Utoaji Huduma katika Masoko ya Mitaji waongezeka
- Hatua Kubwa zafikiwa katika kuvutia Wawekezaji wa Ndani na wa Kimataifa

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameweka alama kubwa ya mafanikio katika maendeleo na ustawi wa sekta ya masoko ya mitaji, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake. Akielezea mafanikio makubwa yaliyopatikana, Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), CPA. Nicodemus Mkama amesema, mafanikio hayo yametokana na mazingira wezeshi na shirikishi ya kisera, kisheria na kiutendaji ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. CPA. Mkama ameongeza kuwa sera za uchumi wa kidiplomasia na uhusiano wa kimataifa zinazotekelezwa chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, zimekuwa chachu yenye matokeo chanya katika kukuza ushiriki wa wawekezaji wa ndani na wa kimataifa na hivyo kuleta mafanikio makubwa zaidi katika masoko ya mitaji. CPA. Mkama amesema, mafanikio yaliyopatikana na ni pamoja na:



*CPA. Nicodemus Mkama Afisa Mtendaji Mkuu, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)*

## Sekta ya Masoko ya Mitaji Imara, Himilivu na yenye mafanikio makubwa

Licha ya uwepo wa athari za janga la UVIKO-19 na migogoro ya kimataifa, masoko ya mitaji nchini yamekuwa salama, himilivu na yenye mafanikio makubwa, ambapo, thamani ya uwekezaji katika masoko ya mitaji imeongezeka kwa asilimia 20.6 na kufikia shilingi trilioni 40.1 katika kipindi kilichoishia Februari 2024, ikilinganishwa na shilingi trilioni 33.3 katika kipindi kilichoishia Februari 2021; Jumla ya mauzo ya hisa na hatifungani yameongezeka kwa asilimia 87.7 na kufikia shilingi trilioni 11.2 katika kipindi kilichoishia Februari 2024, ikilinganishwa na shilingi trilioni 6.0 katika kipindi kilichoishia Februari 2021; na thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja imeongezeka kwa asilimia 297.1 na kufikia shilingi trilioni 2.0 katika kipindi kilichoishia Februari 2024, ikilinganishwa na shilingi bilioni 500.3 katika kipindi kilichoishia Februari 2021.




**Thamani ya Uwekezaji Katika Masoko ya Mitaji Yaongezeka kwa 20.6%**

**Thamani ya Mauzo katika Soko la Hisa Yaongezeka kwa 87.7%**

**Ongezeko la Kuvutia la 297.1% la Thamani ya Uwekezaji Katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

## Tanzania yaweka ALAMA TANO za Kwanza za Mafanikio Kusini mwa Jangwa la Sahara

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza mikakati ambayo imewezesha kuweka ALAMA TANO za Kwanza za Kihistoria za mafanikio Kusini mwa Jangwa la Sahara. Mafanikio hayo ni:

- Utoaji wa hatifungani ya kwanza yenye mguso na matokeo chanya kwa Jamii, iliyotolewa katika fedha mbalimbali, Afrika;
- Utoaji wa hatifungani ya kwanza ya Kijani yenye thamani kubwa iliyotolewa na Kampuni katika fedha mbalimbali, Kusini mwa Jangwa la Sahara;
- Hatifungani ya kwanza yenye mguso wa Jinsia Kusini mwa Jangwa la Sahara;
- Hatifungani ya kwanza inayokidhi misingi ya Shariah yaani Corporate Sukuk bond; na
- Hatifungani ya kwanza ya Kijani ya Taasisi ya Umma kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya Maji na Utunzaji wa Mazingira.

Mafanikio haya yameiweka Tanzania katika ramani ya masoko ya mitaji ulimwenguni yanayotoa bidhaa mpya na bunifu, zinazovutia wawekezaji wa ndani na kimataifa

CPA. Mkama aliongeza kuwa mafanikio makubwa katika masoko ya mitaji nchini ambayo yamechangia kuiweka Tanzania katika ramani ya masoko ya mitaji ulimwenguni yanayotoa bidhaa mpya na bunifu, zinazovutia wawekezaji wa ndani na kimataifa ni pamoja na:



CPA Nicodemus Mkama, Afisa Mtendaji Mkuu, CMSA, akikabidhi hati ya idhini ya toleo la Hatifungani yenye Mguso na Matokeo Chanya kwa Jamii, kwa Bi. Ruth Zaipuna, Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB.

## Hatifungani ya kwanza yenye mguso wa Jamii Afrika

Masoko ya Mitaji Tanzania yameweka historia ya kutoa Hatifungani yenye mguso na matokeo chanya kwa Jamii, iliyoitwa "NMB Jamii Bond", ambapo kiasi cha shilingi bilioni 212.94 kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 284, ikiwa ni toleo la kwanza la Hatifungani yenye thamani ya shilingi za kitanzania Trilioni Moja iliyoidhinishwa na CMSA. Fedha zilizopatikana zinatumika kuendeleza biashara na shughuli za miradi endelevu inayomilikiwa na kuendeshwa na vijana na watu wenye mahitaji maalumu. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa maono na azma ya Mhe. Rais Samia ya uwezeshaji vijana na watu wenye mahitaji maalumu kiuchumi.

## Hatifungani ya kwanza ya kijani Kusini mwa Jangwa la Sahara iliyotolewa katika fedha mbalimbali

Masoko ya Mitaji Tanzania yameweka historia ya kuwezesha utoaji wa Hatifungani ya kijani, iliyoitwa "CRDB Kijani Bond", ambapo kiasi cha shilingi bilioni 171.83 kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 430, ikiwa ni toleo la kwanza la Hatifungani yenye thamani ya shilingi bilioni 780. Fedha zilizopatikana zinatumika kutekeleza biashara na miradi rafiki kwa mazingira. Hatifungani hii ni sehemu ya utekelezaji wa jitihada za Mheshimiwa Rais, za utunzaji wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo akipokea Nakala ya Waraka wa Matarajio wa Hatifungani ya Kijani ya Benki ya CRDB kutoka kwa CPA. Nicodemus Mkama, Afisa Mtendaji Mkuu, CMSA, wakati wa hafla ya uzinduzi wa toleo hilo.



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba anachagiza vyema maendeleo endelevu ya Masoko ya Mitaji katika ukanda wa SADC

## Hatifungani ya kwanza yenye mguso wa Jinsia Kusini mwa Jangwa la Sahara

Masoko ya Mitaji Tanzania yameweka historia ya kuwezesha utoaji wa Hatifungani yenye mguso wa jinsia, iliyoitwa "NMB Jasiri Bond", ambapo kiasi cha shilingi bilioni 74.2 kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 297, ikiwa ni sehemu ya Hatifungani yenye thamani ya shilingi bilioni 200 iliyoidhinishwa na CMSA. Fedha zilizopatikana zinatumika kutoa mikopo kwa ajili ya kuendeleza biashara ndogo na za kati zinazomilikiwa na kuendeshwa na wanawake, pamoja na zile zinazomilikiwa na wanaume lakini bidhaa na huduma zake zina matokeo chanya kwa mwanamke. Hatifungani hii imeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na Soko la Hisa la Luxemburg (LuxLE). Hatifungani hii ni sehemu ya utekelezaji wa azma ya Mhe. Rais Samia ya uwezeshaji wanawake kiuchumi na kukuza usawa wa kijinsia nchini.

## Hatifungani ya kwanza inayokidhi misingi ya Shariah yaani Sukuk bond

Masoko ya Mitaji Tanzania yameweka historia ya kutoa Hatifungani inayokidhi misingi ya Sharia inayoitwa "KCB Fursa Sukuk", ambapo kiasi cha shilingi bilioni 11 kilipatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 110. Fedha zilizopatikana zinatumika kuwekeza katika biashara ndogo na za kati zinazokidhi misingi ya Shariah. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuwezesha uwepo wa bidhaa za aina mbalimbali katika Sekta ya Fedha zinazovutia wawekezaji wa kada mbalimbali, ikiwa ni pamoja na wawekezaji wenye asili tofauti za kimaadili. hivyo kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha.




Bw. Cosmas Kimario, Mkurugenzi Mkuu, Benki ya KCB, kulia, katika uzinduzi wa mauzo ya Hatifungani inayofuata Misingi ya Shariah "Sukuk bond" iliyotolewa na Benki hiyo




Makamu wa Rais wa Jumhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Philip Isdor Mpango, katika hafla ya uzinduzi wa Mauzo ya Hatifungani ya Kijani ya kuendeleza Miundombinu ya Maji na Utunzani wa Mazingira iliyotolewa na Tanga UWASA, tarehe 22 Februari 2024 jiji Tanga. Kulia ni Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso

## Hatifungani ya kwanza ya Kijani ya Taasisi ya Umma kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya Maji na Utunzaji wa Mazingira Barani Afrika

Katika kutekeleza Mkakati wa Serikali wa njia mbadala za kugharamia miradi ya maendeleo katika sekta ya umma na binafsi yaani Alternative Project Financing Strategy, uliozinduliwa na Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Fedha, CMSA imewezesha utoaji wa Hatifungani ya Miaka 10 ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Tanga yaani Tanga Urban Water Supply and Sanitation Authority (Tanga-UWASA) yenye thamani ya shilingi bilioni 53.1 inayowezesha kupata fedha za kutekeleza shughuli za kuboresha miundombinu ya maji na utunzaji wa mazingira. Hatifungani hii ina ubunifu unaojumuisha vipengele vinavyogusa taasisi ya umma, ujenzi wa miundombinu ya huduma endelevu za maji, utunzaji wa mazingira na miradi yenye uwezo wa kujiendesha kibiashara na inaweka msingi madhubuti wa kuonyesha njia kwa Taasisi za umma; na Mamlaka za Serikali za Mitaa namna ya kupata fedha za kugharamia miradi yenye uwezo wa kujiendesha kibiashara, kupitia masoko ya mitaji.

# Wataalamu na Taasisi zenye weledi na ujuzi kwa ngazi ya kimataifa waongezeka

CPA. Mkama pia alibainisha kuwa, katika Kipindi cha miaka mitatu ya Mhe. Dkt. Samia, CMSA ilitekeleza mikakati mbalimbali iliyowezesha kuongezeka kwa wataalamu wenye weledi na sifa zinazotambulika kimataifa; kuongezeka kwa leseni zilizotolewa kwa kampuni zinazotoa huduma katika masoko ya mitaji; na kuzinduliwa kwa mpango wa mafunzo endelevu kwa watalaamu na watendaji katika masoko ya mitaji:




*Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Hamad Hassan Chande akikabidhi cheti kwa mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya ngazi ya kimataifa ya watendaji wa Masoko ya Mitaji, wakati wa mahafali ya mafunzo hayo. Kushoto ni CPA Nicodemus Mkama, Afisa Mtendaji Mkuu, CMSA.*

## Wataalamu wa Masoko ya Mitaji Wanaotambulika Kimataifa waongezeka kwa 61.5%

Katika jitihada za kuongeza wataalamu wenye weledi na ujuzi kimataifa kwenye masoko ya mitaji, CMSA kwa kushirikiana na Taasisi ya Uwekezaji na Dhamana ya nchini Uingereza yaani Chartered Institute for Securities and Investment (CISI) imetoa mafunzo yanayotambulika kimataifa kwa watendaji wa masoko ya mitaji hapa nchini. Mafunzo haya yamewezesha kujenga uwezo na ufanisi kwa watendaji wa masoko ya mitaji katika ngazi ya kimataifa, ambapo idadi ya wataalamu wanaokidhi viwango vya kimataifa imeongezeka kwa asilimia 61.5 na kufikia 798 katika kipindi kilichoishia Februari 2024 kutoka 494 katika kipindi kilichoishia Februari 2021. Mafunzo haya yamewapatia wataalamu wa masoko ya mitaji fursa ya kupata leseni za kutoa huduma katika masoko ya Kitaifa, Afrika Mashariki na kimataifa. Hatua hii imewajengea uwezo wataalamu wa masoko ya mitaji kuanzisha bidhaa bunifu katika Masoko ya Mitaji nchini.

## Uzinduzi wa Mpango wa Mafunzo Endelevu kwa Wataalamu wa Masoko ya Mitaji

CMSA imezindua mpango wa mafunzo endelevu kwa wataalamu wa masoko ya mitaji yaani Continuous Professional Development Program (CPD) wenye lengo la kuhuisha uelewa na kujenga uwezo wa watalamu hawa kuhusu mabadiliko, changamoto za maendeleo na masuala yanayoibuka siku kwa siku katika nyanja za masoko ya mitaji nchini na ulimwenguni kote. Mafunzo endelevu ni muhimu kwa udhibiti wa Soko na kulinda maslahi ya wawekezaji katika masoko ya mitaji kwani itawajengea ujuzi wa kudhibiti viashiria vya hatari vinavyoweza kujitokeza katika masoko ya mitaji. Hatua hii ni muhimu katika kutekeleza Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wenye lengo la kujenga uwezo wa rasilimali watu katika Sekta ya Fedha.





*Kamishana wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Wizara ya Fedha Dkt. Charles Mwamaja akifungua pazia ikiwa ni ishara ya uzinduzi wa Mpango wa Mafunzo Endelevu ya Watendaji wa Masoko ya Mitaji (CPD), na kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya CMSA Dkt. John Mduma. Kulia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, CPA. Nicodemus Mkama, akifuatiwa na Mwakilishi wa Taasisi ya CISI, Bw. Christopher Morris.*



*CPA. Nicodemus Mkama, Afisa Mtendaji Mkuu wa CMSA akitoa mada wakati wa mkutano wa Wadau wa Masoko ya Mitaji*

## Kampuni zenye Leseni ya Kutoa Huduma katika Masoko ya Mitaji zaongezeka kwa 27.8%

Utekelezaji wa mafunzo kwa watendaji wa masoko ya mitaji yanayotambulika kimataifa yamewezesha idadi ya watendaji wa masoko ya mitaji wenye leseni ya CMSA kuongezeka kwa asilimia 27.8 na kufikia 184 Februari 2024 kutoka 144 Februari 2021. Kuongezeka kwa idadi ya watendaji wa masoko ya mitaji ni hatua muhimu katika kuwezesha utekelezaji wa Mpango wa tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wenye lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma rasmi za fedha kwa wananchi.



## Elimu ya Fedha na Uelewa wa Masoko ya Mitaji waongezeka

Katika jitihada za kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu fursa zinazopatikana katika masoko ya mitaji, CPA. Mkama amesema, CMSA imebuni, kuboresha na kutekeleza mikakati mbalimbali ya utoaji wa elimu kwa umma. Mikakati hiyo ni pamoja na:



*Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Hamad Hassan Chande akikabidhi zawadi kwa Washindi wa Shindano la Masoko ya Mitaji kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Elimu ya Juu, Oktoba 2024*

### Kuendesha Mashindano kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Taasisi za Elimu ya Juu

CMSA imeendesha mashindano kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kuhusu masoko ya mitaji na uwekezaji. Mashindano hayo yameonyesha mafanikio makubwa kutokana na kuendeshwa kwa kutumia njia ya mitandao ya kielektroniki yaani simu za mikononi na intaneti. Mashindano haya yamesaidia kuongeza elimu ya masoko ya mitaji kwa vijana wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu, ambapo idadi ya washiriki imeongezeka na kufikia wanafunzi 88,871 katika kipindi kilichoishia Februari 2024 kutoka wanafunzi 48,662 katika kipindi kilichoishia Februari 2021, ikiwa ni ongezeko la asilimia 82.6. Mashindano haya yamekuwa na matokeo chanya kwa kuongeza idadi ya wawekezaji vijana 10,000 katika masoko ya mitaji;



kuanzishwa kwa Jukwaa la Wawekezaji Vijana lenye wanachama zaidi ya 6,000 ambalo linawezesha wawekezaji vijana kupata elimu na uzoefu wa uwekezaji katika masoko ya mitaji. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa maono na azma ya Mhe. Rais Samia ya uwezeshaji vijana kiuchumi.

*Washindi wa Shindano la Masoko ya Mitaji kwa Wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Elimu ya Juu wakipewa maelezo kutoka kwa Afisa wa UTT AMIS, wakati wa ziara ya mafunzo kwa Washindi wa shindano hilo.*

# Programu za Utoaji wa Elimu kwa Umma

CMSA imetekeleza programu mbalimbali zenye lengo la kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji. Programu hizo zimetolewa kwa makundi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vijana, vikundi vya wanawake, wajasiriamali, watunga sera, waheshimiwa wabunge, taasisi za umma na binafsi, makundi ya kijamii na watu wenye mahitaji maalumu.




*Bi. Adella Kaale, Meneja wa Masuala ya Sheria na Ufuatiliaji wa CMSA, akitoa mada wakati wa semina za elimu kwa umma kuhusu uwekezaji katika mfumo wa Mitaji Halaiki "Crowdfunding platforms"*

# Kushiriki katika Maonyesho

CMSA imeshiriki katika maonyesho ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kutoa elimu kuhusu fursa na faida zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji, ikiwa ni pamoja na Wiki ya Wawekezaji Duniani; Wiki ya Huduma za Fedha; na Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba, Maonyesho ya Kimataifa ya Wakulima



*Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha akipokea maelezo kuhusu mwenendo wa sekta ya masoko ya mitaji kutoka kwa watumishi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) wakati wa ziara yake kwenye Maonyesho ya 46 ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba.*




*Maafisa kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, walioshiriki katika maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha jijini Arusha Novemba 2023, wakifurahia Tuzo ya mhamasishaji bora katika maadhimisho hayo.*



*Afisa Mwandamizi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana akipokea maoni kutoka kwa mmoja wa wadau wa soko la mitaji na dhamana wakati wa mkutano kati ya Mamlaka na wadau.*

# Kuongezeka kwa Ufanisi wa Masoko ya Mitaji

CPA. Mkama pia ameeleza kuwa jitihada mbalimbali zimechukuliwa katika ili kuongeza ufanisi katika masoko ya mitaji. Jitihada hizo ni pamoja na:



# Kuimarisha Ushiriki wa Wawekezaji wa Ndani katika masoko ya mitaji




*Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dkt.Natu El-maamry Mwamba akitoa hotuba wakati wa uzinduzi wa Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa Faida ulioidhinishwa na CMSA.*

Katika kuimarisha ushiriki wa wawekezaji wa ndani katika masoko ya mitaji, CMSA imetekeleza mkakati ambao Umewezesha kuanzishwa na kuidhinishwa kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja unaoitwa Faida Fund, unaoendeshwa na Taasisi ya Watumishi Housing Investments (WHI). Mauzo ya awali ya Mfuko huu yamewezesha kupatikana kiasi cha shilingi bilioni 12.95, ikiwa ni mafanikio ya asilimia 173. Mfuko huu unatoa fursa ya kuwekeza kwa kuanzia shilingi 10,000 hivyo kuwezesha wawekezaji wa kada mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vijana, wanawake, makundi maalum kunufaika na uwekezaji katika masoko ya fedha; kujenga utamaduni wa kuweka akiba; na kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi. Kuanzishwa kwa Mfuko huu ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha, ambao pamoja na mambo mengine una lengo la kuongeza idadi ya bidhaa bunifu na zenye gharama nafuu katika ushiriki katika Sekta ya Fedha.

# Hatua Kubwa katika kuvutia Wawekezaji wa Kimataifa

Tanzania imetekeleza mageuzi makubwa katika kuweka mazingira wezeshi ya ushiriki wa wawekezaji wa kimataifa (Free Movement of Capital). Kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia kuhusu tathmini ya Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani East African Common Market Protocal Scorecard on Movement of Capital, Tanzania imepanda viwango vya alama za tathmini kwa asilimia 157 kutoka alama 7 hadi alama 18 kati ya 20 katika utekelezaji wa itifaki ya soko la pamoja katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa sasa, Tanzania hakuna vikwazo vya ushiriki wa wawekezaji wa kigeni katika soko la hisa, hatifungani za kampuni na mifuko ya uwekezaji wa pamoja, hatua hii inafanya Tanzania kuwa kivutio muhimu kwa wawekezaji wa kimataifa.

# Kuongeza Ushiriki wa Wawekezaji kupitia Matumizi ya Teknolojia

Katika kuwezesha matumizi ya teknolojia ili kuongeza ushiriki wa wawekezaji katika masoko ya mitaji, CMSA imewezesha matumizi ya mifumo ya Sim Invest na Hisa Kiganjani ambayo inawezesha kutoa huduma katika masoko ya mitaji kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika kuuza na kununua dhamana. Hatua hii imewezesha kuongeza ushiriki wa wananchi mijini na vijijini katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja na soko la hisa. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa tatu wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wenye lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma rasmi za fedha kwa wananchi mijini na vijijini.









CPA. Mkama amehitimisha kwa kusema kuwa, Sekta ya Masoko ya Mitaji Tanzania ni imara na himilivu na kuwa CMSA itaendelea na jitihada zenye lengo la kuchagiza na kutoa mchango chanya katika kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya watu. CPA. Mkama amemtakia Mheshimiwa Rais Dk. Samia heri katika uongozi wake na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema, baraka na fanaka katika kutekeleza kazi ya kuleta maendeleo ya jamii na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.